**MASWALI NA MAJIBU: KUHAKIKISHA USALAMA WA CHAKULA KWA WOTE**

Amira Dauod Hassan Gornasss, Balozi wa Jamuhuri ya Sudani, nchini Italia na Mwakilishi wa Kudumu wa Jamuhuri ya Sudani katika Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa Mjini Rome, anachukua jukumu lake kama Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (Committee on World Food Security –CFS), Amira anatueleza maono yake kuhusu usalama wa chakula katika siku zijazo.

**Rome, Italia, Januari 19, 2016 (IPS)-** Kwa kuwa ninatoka katika nchi inayoendelea ambapo, katika kizazi chetu, tumeshuhudia athari kubwa za ukosefu wa usalama wa chakula na ugumu wa kuelewa vyanzo vya ukosefu wa usalama wa chakula, ninalichukulia lengo la kuhakikisha kwamba wakati wa uongozi wangu kama Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani nitaleta mabadiliko 'yanayooenekana" katika maisha ya watu. Kuafikia matokeo ni jambo ambalo tunahitaji kutimizia kila mmoja wetu na kila mtu aliye na utapiamlo ambaye leo, katika mwaka wa 2016 anaenda kulala na njaa bila kula chochote. Kunayo idadi isiyokubalika ya watu milioni 793 wanaoenda kulala bila chakula na wenye utapiamlo duniani kote! Kuhakikisha kuwa kuna usalama wa chakula kwa wote ni jukumu ambalo tunahitaji kutimizia watoto wetu.



**Mheshimiwa Amira Daoud Hassan Gornass, Balozi wa Jamuhuri ya Sudani, Nchini Italia na Mwakilishi wa Kudumu wa Nchi ya Sudani katika Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa mjini Rome, Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (CFS) – Picha ni kwa hisani ya: CFS**

Leo hii katika ulimwengu wa Karne ya 21 wenye uhusiano wa karibu, uwepo wa njaa na utapiamlo usioisha ni jambo ambalo halikubaliki na jambo gumu kushulighulikia. Vyanzo asili vya hali hii ni vingi, na vina uhusianio wa karibu, na vitashughulikiwa tu kikamilifu ikiwa wadau wote wakijumuisha, serikali, jamii ya kiraia, sekta ya kibinafsi, Mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN) na jumuiya ya kimataifa ya maendeleo kwa jumla pamoja na mashirika ya utafiti, watakuja pamoja na kukubaliana kuhusu sera na hatua zinazohitajika ili kushughulikia suala la njaa na utapiamlo. Hii ndio sababu Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (CFS), ni jukwaa jumuishi kabisa la wadau wote kufanya kazi kwa pamoja kukumbana na ukosefu wa usalama wa chakula na kubuni sera za lishe bora duniani kote. Kamati hii imepewa jukumu kuu katika kushughulikia maeneo mawili: utekelezaji wa Ajenda ya mwaka wa 2030 ya Maendeleo Endelevu na mapendekezo ya Kongamano la Pili la Kimataifa kuhusu Lishe.

Ukaguzi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Ajenda ya Mwaka wa 2030, na hasa lengo la pili la, "Kukomesha njaa, kuafikia usalama wa chakula na lishe bora na kukuza kilimo cha kudumu", na pia hatua za kumaliza kabisa utapiamlo katika hali zake zote, utahitaji majukwaa ambayo yanaweza kuhakikisha ujumuishaji, mwingiliano wa sera za sayansi zifaazo, na mwelekeo unaohakikisha kwamba hifadhi ya vyakula imejaa.

Shukrani kwa ripoti faafu kutoka kwa Kamati ya Wataalamu Wakuu na pia wadau tofauti tofauti walioshiriki katika kuandaa ripoti hizi, Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (CFS) yenye uhalali na umiliki mpana, inajadili vifaa vya kisera kulingana na maarifa na ushahidi uliopo. Hatuwezi kuendelea kushikilia kwamba tuna upungufu wa uelewa na maarifa kuhusu athari za vitendo vyetu, na leo hii, lazima watu wote wawajibikie hatua na chaguo zao.

Uwajibikaji ni kipaumbele ambacho nimejiwekea kama mwenyekiti wa Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (CFS) katika miaka miwili ijayo. Hali ya mwanadamu inaendelea kubadilika na Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (CFS) lazima iwe tayari kubadilika ili iwe jumuishi, yenye uwazi, yenye utendakazi na ifaayo kutimiza mabadaliko duniani. Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (CFS) lazima iendelee kujiuliza maswali kwa njia itakayoleta manufaa, na kuchunguza ikiwa hatua zake ni faafu, ikiwa kamati yenyewe ni jumuishi kama inavyotakikana, ikiwa ripoti zinazoegemea zaidi sayansi zinaunga mkono majadiliano ya kisera kadri iwezekanavyo na maswali mengi zaidi. Mwaka huu, tunapanga kuendeleza tathmini huru ya Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (CFS), na tunayatarajia matokeo ya tathmini hii ili tuweze kuendelea na mabadiliko na uboreshaji wa Kamati.

Vipaumbele hivi vinawakilisha mabadiliko katika Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (CFS) na kwa uhakika vipaumbele vitajumuisha changamoto na pia fursa za kuthibitisha kwamba mfumo shirikishi na jumuishi kama ule wa Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani )(CFS) ndio mfumo wa maendeleo endelevu katika siku zijazo. Ninatarajia kwamba miaka hii miwili, tukishirikiana na wadau wote wa Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (CFS) tutaafikia athari za kudumu.

Yafuatayo ni mahojiano yaliyofanywa na IPS na Balozi Gornass

*IPS: Tafadhali tueleze baadhi ya changamoto ngumu mno ambazo tunakumbana nazo katika hatua za kuafikia Kutokuwa na Njaa kamwe duniani kote.*

*Balozi Gornass*: Sayari yetu kadri ilivyo kubwa na yenye mengi, ina mipaka na rasilimali asilia chache. Rasilimali hii, ambayo siku hizi katika ulimwengu wenye idadi kubwa ya watu na utangamano mkubwa, inaendelea kupunguka zaidi. Hali hii imechangia katika kupigania mashamba, maji, lishe miongoni mwa rasilimali nyingine Virutubishi vya udongo ardhini vinaendelea kudidimia. Hii imeleta athari kubwa katika uzalishaji katika kilimo, na athari zaidi katika mazingira yetu. Mabadiliko katika hali ya anga ndio jambo moja linalotatanisha miongoni mwa baadhi ya mabadiliko ambayo yanatuathiri sisi sote bila chaguzi zozote. Sababu za kisiasa na za serikali pia zinachangia katika hali hii duniani, migogoro ya mabadiliko ya hali ya anga inaendelea kuongezeka. Migogogo hii inaathiri uzalishaji wa chakula kutoka hatua ya mwanzo ya kulima hadi hatua ya kuvuna na hatimaye hatua ya kuchakata mazao. Hatua za ugavi wa chakula na hatua ya mwisho ya kumfikia mtumizi wa chakula pia zinathirika. Mojawapo ya suala kuu linaloathiri usalama wa chakula na lishe ulimwenguni kote ni suala la ushirikiano na uwiano katika uundaji sera. Kwa mfano, wizara kadhaa katika serikali huenda zisiwe na maoni sawia au huenda hata zikawa na maoni tofauti na wakati mwingine mielekeo shindani ya kushughulikia suala, mara nyingine wizara haziamini hatua zake. Nchi zilizo katika eneo moja lazima ziborehse ushirikiano wake wa kisera. Jambo lingine tunalohitaji kuafikiwa ni mawasiliano bora baina ya nchi hizi.

Kijumla, ni muhimu kuwepo kwa ufahamu kutoka kwa wadau wote kuhusu majukumu yao: kila mdau ana jukumu na wajibu katika kuafikia usalama wa chakula na kuboresha lishe.

*IPS: Kufikia sasa ni wapi tumefanikiwa na ni kipi kitachofanya kazi zaidi katika kukumbana suala la usalama wa chakula? Je, lengo la Pili katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG2) la lengo la kutarajiwa tu au kwa kweli tunaweza kulitimiza kufikia mwaka wa 2030?*

*Balozi Gornasss*: Kuna baadhi ya mifano ya maendeleo makuu katika hatua za kukumbana na njaa. Duniani kote, idadi ya watu wanaoathiriwa na njaa inaendelea kupunguka na kwa jumla maeneo yanaendelea kuonyesha maendeleo mema, huku maeneo fulani yakiwa yameafikia malengo ya kimataifa ya mwaka wa 2015 ya mapambano dhidi ya njaa na kuwepo kwa lishe bora. Hata hivyo, maeneo mengine kwa kweli yamerudi nyuma kutokana na athari mpya hasa zile za migogoro ya kisiasa.

Kwa kweli, Lengo la Pili katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG2) laweza kuafikiwa kufikia mwaka wa 2030.Tayari tunajua namna ya kuzalisha chakula cha kutosha cha kulisha watu wote duniani. Kwa sasa, ni muhimu kuelewa namna mifumo ya chakula inaweza kufanya kazi bora zaidi ili tusipoteze au kuharibu chakula, kwamba ugavi wa chakula udhihirishe usawia, chakula kipatikane kwa bei nafuu ambayo inawezesha wazalishaji chakula kuboresha maisha yao na kuhimizwa kuzingatia kazi zilizopo katika sekta ya kilimo, na kwamba mifumo hii ijumuishe lishe bora na inayotosheleza. Matokeo yake yatakuwa kwamba watu wataweza kuishi vyema zaidi na nchini zitaweza kukua zaidi. Kuongeza uzalishaji chakula wa wakulima wadogo wadogo ni muhimu katika kuafikia haya. Kijumla, wakulima hawa wadogo ndio watu watakaoleta mabadiliko katika lishe na hali ya ubora wa chakula.

*IPS: Je, unaweza kutoa baadhi ya mifano mahususi ya mafanikio na pia utueleze mwelekeo unaohitajika katika siku zijazo katika nchini nyinginezo?*

*Balozi Gornass*: Brazili ni mfano mzuri. Kwa mfano Programu ya ‘Zero Hunger’ ya Rais wa Awali, Rais Lula. Programu hii ya serikali ya Brazili iliyoanzishwa na Rais Luiz Inácio Lula da Silva, ni programu yenye lengo la kukomesha kabisa njaa na umaskini uliokithiri kwa kuunganisha baadhi ya sera za ulinzi wa kijamii na mbinu za kisalama kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa wakulima wadogo wadogo.

India, vilevile, ina mafanikio mengi tunayoweza kueleza! Kwa mfano, Nchi ya India ilianzisha kampeini ilioonyesha mafanikio makuu, kampeini hii ilikuwa ya mitandao ya kijamii iliyonuiwa kuelimisha watu wote – na hasa ikilenga wanawake – kuwaelimisha kuhusu ishara na athari za utapiamlo, pia manufaa ya mlo kamili wenye virutubishi kutoka makundi yote ya vyakula, hasa kwa watoto wachanga na watoto wanaokua chini ya umri wa miaka tano. Kampeini hii ilianzishwa na kuungwa mkono na kampuni ya simu, ambayo iliwapa dakika zaidi za simu watu walioona video ya maelezo iliyotolewa. Kutokana na kampeini hii, idadi ya watu wanaougua kutokana na utapiamlo ilipunguka kutoka asilia 51 hadi asilimia 37!

*IPS: Kuafikia usalama wa chakula kunaweza kutatua mambo mengi ikiwa ni pamoja na kwa mfano kupunguza masuala ya afya ambayo katika kiwango cha kitaifa yanasababisha ugumu kwa uchumi wa taifa, bila hata kuzingatia athari kwa mtu anayeugua kutokana na ukosefu wa chakula na utapiamlo. Je, unafikiria kwamba viongozi wa mataifa ya dunia wanaelewa umuhimu wa usalama wa chakula?*

*Balozi Gornass*: Ndio, wanaelewa! Huu ni ujumbe ambao ulizungumziwa mwezi wa Septemba mwaka uliopita wakati wa kuidhinishwa kwa Ajenda ya mwaka wa 2030 ya Maendeleo Endelevu; masuala ya maendeleo yana uhusiano wa karibu na tunahitaji kushughulikia masuala haya kwa pamoja, kwa njia kamilifu na jumuishi, tukileta pamoja: nchi zinazoendea na nchi zilizoendelea; serikali, na wadau wengine wote.

Changamoto ni kwamba, huku usalama wa chakula na lishe bora huleta manufaa ambayo yanaathiri sekta kadhaa, kama vile afya, ukuaji wa uchumi kama ulivyotaja, pia mazingira na kwa jumla uzima wa idadi nzima ya watu, kuafikia hili kunahitaji kutekelezwa kwa mambo kadhaa kwa pamoja miongoni mwa sekta tofauti. Kwa mfano, “sera zinazozingatia lishe” lazima zijumuishwe katika mipango ya afya, programu za maendeleo ya kilimo, usimamizi wa maji, elimu, na kadhalika. Katika hali hii usalama wa chakula na lishe utaafikiwa tu ikiwa wadau wote watatambua haya na kufanya kazi kwa pamoja. Hii ndio pia sababu Ajenda ya mwaka wa 2030, na lishe iliyoboreshwa, vitapewa nafasi kuu kwenye Ajenda ya Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (CFS) kuanzia sasa; wanachama wa Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani ambao ni wadau watakutana mwaka huu katika Makundi Wazi ya Utendakazi ili kujadili jinsi ya kutekeleza maamuzi yaliyochukuliwa katika Mkutano wa Kijumla wa Kamati mnamo mwezi wa Oktoba 2015.

*IPS: Je, mabadiliko katika hali ya anga ni changamoto kubwa katika kuafikia usalama wa chakula na kutokuwepo kwa njaa kufikia mwaka wa 2030? Ikiwa hatufahamu mabadiliko ya hali ya anga tutawezaje kusonga mbele kuafikia usalama wa chakula? Je, ni jukumu lipi Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (CFS), imechukua kushughulikia suala hili na Je, kamati hii inaweza kuchukua jukumu kubwa zaidi katika mabadiliko ya hali ya anga?*

*Balozi. Gornass*: Kwa kweli, mabadiliko ya hali ya anga yana athari kubwa, hasa katika nchi zinazoendelea. Ongezeko la digrii mbili kwenye viwango vya joto litakuwa na athari kubwa kwa mazao na viwango vya virutubishi

katika mazao kutoka maeneo mengi ya dunia. Ongezeko hili litaathiri mabadiliko ya anga ambayo matokeo yake yatakuwa ni athari kali mno kwa mavuno na uwepo wa chakula.

Mabadiliko ya hali ya anga pia huenda yakachangia katika ongezeko la watu waliokosa makazi, “wakimbizi wa kimazingira” ongezeko hili lina athari kubwa kwa usalama wa chakula. Mabadiliko madogo katika hali zenye mshikamo usio thabiti yanaweze kuwa na athari za kisiasa na kibinadamu. Nchi zote zinahitaji kufanya kazi kwa pamoja ili kubadilisha na kudhibiti mabadaliko ya hali ya anga: tunahitaji kushughulikia zaidi utoaji wa usaidizi wa kifedha na kiufundi. Pia tunahitaji kuwawezesha wakulima kuweza kudhibiti mabadiliko haya ya hali ya anga. Tunahitaji kutafuta na kutumia mbinu za uzalishaji kilimo zinazoweza kudumu na hili lifanywe kwa haraka. Lakini pia njia za kutatua mabadiliko ya hali ya anga zinaweza kufikiwa, kutokana na uwezo wa teknolojia na uvumbuzi, na maarifa ya kijadi miongoni mwa jamii mbalimbali ya namna ya kuzalisha chakula chenye ubora huku matumizi ya rasilimali iliyopo yakizingatiwa kwa uwezo wake kamili na kwa njia inayoweza kudumu.

Kuhusiana na suala hili, Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (CFS), imeidhinisha ripoti ya Jopo la Watalaamu Wakuu, ripoti hii inajulikana kama “Maendeleo Endelevu ya Kilimo Yakijumuisha Majukumu ya Kilimo cha Wanyama wa Nyumbani - Sustainable Agricultural Development Including the Role of Livestock”, ripoti hii itazinduliwa mnamo Julai, 2016. Katika mwaka wa 2012, Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (CFS), ilichapisha ripoti inayojulikana kama, “Mabadiliko ya Hali ya Anga na Usalama wa Chakula,” ripoti hii ina uwezo wa kuleta mabadiliko muhimu. Ripoti hii inatanguliza dhana ya “Kilimo Kinachozingatia Mabadiliko ya Hali ya Anga” huku ripoti hii ikijumuisha majadiliano kwamba kilimo na mahitaji ya kilimo lazima yajumuishwe katika majadiliano yoyote kuhusu hali ya anga- kwamba kilimo sio tu sehemu la tatizo lakini kwamba kilimo kinachozingatia Mabadiliko ya hali ya anga kina uwezo mkubwa wa kuzalisha utatuzi wa matatizo ya mabadiliko ya hali ya anga! Mapendekezo ya kisera ambayo yalijadiliwa kulingana na ripoti hii yangali katika majukwaa ya kimajadiliano kuhusu mabadiliko ya hali ya anga.

Katika hali ya kuweza kufikia COP 21, Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (CFS) kwa uwazi imetetea kwamba mwelekeo wa kuzingatiwa duniani kote wa maendeleo endelevu kubuniwa katika miaka 15 ijayo- mwelekeo huu ujumuishe Malengo ya Maendeleo, Ufadhili wa Maendeleo, na hatua za haraka za kushughulikia mabadiliko ya hali ya anga- huku mwelekeo huu ukihakikisha kwamba wadau wote wanachukua jukumu lao kikamilifu na kuchangia katika dunia bora zaidi.

Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani itaendelea kutumia mfumo wake, kufanya kazi na kuwaleta pamoja washika uongozi kuunga mkono hatua za pamoja, huku kamati hii ikihakikisha kwamba utekelezaji wa Malengo yote ya Maendeleo Endelevu ambayo yapo katika majukumu yake unazingatia mahitaji ya kujumuisha hatua za kubadili hali ya mabadiliko ya hali ya anga.

Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani (CFS) inajitolea kuunga mkono wadau wote katika ujenzi wa dunia ambayo kufikia mwaka wa 2030 hakuna mwanadamu yeyote aliyewachwa nyuma kimaendeleo.